TANGAZO LA SERIKALI NA. 79 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KAKOLA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Kakola ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 126 yenye majira-nukta 427830MS, 9626462KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS133$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 1.65 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 127 yenye majira-nukta 428448MS, 9624924KZ; baada ya hapo

mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS121$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 7.37 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 131 yenye majira-nukta 437134MS, 9623533KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ96$^{0}$KZ kwa umbali wa kilomita 3.88 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 132 yenye majira-nukta 437858MS, 9627347KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS255$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 8.40 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 136 yenye majira-nukta 446639MS, 9627784KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ106$^{0}$KZ kwa kukatisha mto Bulyanhulu kwa umbali wa kilomita 8.70 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 121 yenye majira-nukta 449043MS, 9638154KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ152$^{0}$MG kwa umbali wa klomita 4.49 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 254 yenye majira-nukta 448094MS, 9640543KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS81$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 3.73 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 253 yenye majira-nukta 444621MS, 9639167KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ243$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 2.40 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 255 yenye majira-nukta 442818MS, 9640765KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS318$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 3.00 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AID 407 yenye majira-nukta 445993MS, 9640795KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ119$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 3.01 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 258 yenye majira-nukta 447436MS, 9643439KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG67$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 8.60 kukatisha mto Bulyanhulu hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 256 yenye majira-nukta 438893MS, 9644322KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG163$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita kukatisha mto Bulyanhulu hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 234 yenye majira-nukta 438064MS, 9644163KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG132$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 15.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba SHV 125 yenye majira-nukta 430127MS, 9631298KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS174$^{0}$MG kwa umbali wa kilomita 5.35 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*